# Hatua za Kiutendaji za Kuwafuasa Wanafunzi

Kutoka kwa Mfululizo: Hatua Kuelekea Ukomavu

KUMFUATA YESU
KUTUMIA WAKATI PEKE YAKO NA MUNGU
KUMFANYA YESU KUWA BWANA
KUISHIRIKI IMANI YAKO
KUUATHIRI ULIMWENGU WAKO



Barry St.Clair

# Hatua za Kiutendaji za Kuwafuasa Wanafunzi

Ninapowatayarisha watu kuwafuasa wengine, ninapenda kuuliza, “Je, unaweza kusoma?” Ukiweza, unaweza kuongoza kikundi cha uanafunzi. Mara nyingi mimi huyafanya mambo rahisi kuwa magumu sana. Lakini Mungu ana ustadi wa ajabu wa kuyarahisisha mambo kwa ajili ya watu kama mimi.

Kuanzisha kikundi cha uanafunzi, fuata hatua hizi zilizo wazi, za vitendo.

1. **Omba**. Hatua hii inatumika kama ukumbusho kwamba bila uwepo wa Mungu na nguvu hatutimizi chochote cha thamani ya milele. Alika uwepo na nguvu za Mungu katika kila jambo unalofanya. (Angalia sehemu ya kwanza ya kitabu changu cha *Kuwapasha Wazazi*, Sura ya 10 kwa baadhi ya matumizi ya vitendo.)

2. **Chagua**. Muulize Bwana, “Unataka nani katika kundi hili—ni nani aliye wazi na ana njaa ya kukujua Wewe?” Mara tu unapopata mwelekeo fulani juu ya swali hili, kutana na kila mtu kibinafsi. Katika mkutano huo wape changamoto kali.

3. **Tia Changamoto**. Baadhi ya watu wanaogopa kuwaalika wengine kujiunga nao katika tukio la kuwafuasa wanafunzi. Hiyo inaeleweka, lakini aina hiyo ya woga haitoki kwa Mungu. Unaweza kufikiria sababu nyingi kwa nini mtu huyo hataki kufanya hivi. Yakatae mawazo hayo.
   Toa changamoto kwa kila mtu kufuata maono ya Mungu kwa maisha yake. Fungua Biblia yako kwenye Mathayo 4:19, mtazame huyo mtu mwingine machoni, na useme, “Ninaona uwezo wa Mungu ndani yako.  Mungu ana kusudi kubwa sana kwa maisha yako. Ninataka kukusaidia kugundua jinsi ya kumfuata Yesu na kuwavua watu.  Ndio maana nakutaka katika kundi hili.”

4. **Kujitolea**. Mara tu unapompa changamoto kila mtu kibinafsi, kutaneni kama kikundi. Katika hali ya utulivu jadili masuala yafuatayo:

   - Gharama: “Tutakutana saa moja kila _______ saa _____. Ninakuomba ulipie gharama hii ili ujiunge na kikundi hiki. Ukijitolea, utahitaji kuhudhuria kila juma na kufanya migawo yote kila juma.”

   - Faida: “Kikundi hiki kitakusaidia kuwa mwanamume/mwanamke wa Mungu. Utapiga hatua kuelekea ukomavu katika Kristo na utakuwa kiongozi anayesaidia wengine kumjua Kristo.”

- Ahadi: Mpe kitabu cha *Hatua Kuelekea Ukomavu*. (Ona orodha iliyo hapa chini.) "Chukua kitabu hiki. KItatuongoza kila wiki. Kama sehemu ya ahadi yetu, lazima uje ukiwa tayari. Fungua ukurasa wa 11 katika *Kumfuata Yesu* [au kitabu kingine cha *Hatua Kuelekea Ukomavu*], ili tuweze kuelewa kwa uwazi ahadi zetu sisi kwa sisi." Kisha wakati wa mikutano miwili au mitatu ya kwanza ya vikundi, soma tena ahadi kila mara. Waulize watu tofauti wasome kila nukta. Kisha waambie wote watie sahihi kitabu cha kila mmoja wao kwenye ukurasa wa 11 kama ahadi ya kujitolea kwa kikundi na kwa kila mmoja wao. Kwa kufanya hivi wanafahamu uzito wa kujitolea kwao.

- Malipo: Waulize kulipia kitabu. Hii inawasaidia kutambua kuwa kuwa sehemu ya kikundi kutawagharimu kitu...

5. **Tayarisha**. Kabla ya kundi kukutana mara ya kwanza mambo kadhaa yanahitajika kutendeka ili mje mkiwa tayari.

   - Tazama kikundi kama mchakato wa muda mrefu—tunatumai utawafanya watu hawa kuwa wanafunzi kwa njia fulani katika maisha yako yote! Na pia kuna uwezekano utafanya kazi na kikundi hiki katika miaka michache ijayo.

   - Tumia vitabu vya *Hatua Kuelekea Ukomavu* kwa mtazamo wa mchakato wa muda mrefu. Msururu wa Kusonga kuelekea Ukomavu, vitabu vitano vya majuma kumi kila kimoja, vitakupeleka kwenye hatua ya kulikomaza kundi lako katika Kristo. Kila kitabu kimejengwa juu ya kile kilichotangulia.

*Kumfuata Yesu* hujenga msingi thabiti wa uhusiano wa kubadilishiwa maisha na Kristo na kwa kuwa mfuasi wa Kristo.

*Wakati Peke Yako na Mungu* huimarisha uhusiano wa kila mtu na Yesu kwa kufundisha jinsi ya kutumia muda pamoja Naye.

*Kumfanya Yesu Bwana* ni changamoto kwa kila mtu kumtii Yesu na kumpa mamlaka katika masuala ya kila siku.

*Kuishiriki Imani Yako* humwongoza kila mtu kwenye adhama ya kushinda hofu yake na kuchukua hatari ya kuwasiliana na Kristo kwa ujasiri.

*Kuuathiri Ulimwengu Wako* huonyesha washiriki wa kikundi kwamba wanaweza kuwa viongozi wenye ushawishi kupitia kuhudumia mahitaji ya watu wanaowazunguka.

Vitabu vitatu vya ziada vitasaidia mchakato wa kuwafuasa wanafunzi.

*Mwongozo wa Kiongozi Hatua Kuelekea Ukomavu,* ambao unasoma sasa, utakuongoza kuongoza kundi lako. Hapa una muundo rahisi wa kuongoza kikundi hai cha ufuasi na kinachobadilisha maisha.

*Daftari la Wakati Peke Yako na Mungu* linatoa zana za vitendo kwa ajili ya matukio ya kila siku na Mungu.

*Kuanza* huwasaidia waumini wapya kuanza kwa mafanikio kutembea na Kristo.

Kusoma na kupitia vitabu hivi itachukua miaka miwili au zaidi. Ikiwa kikundi chako ni vijana wachanga, na unaanza wakati watoto wako wanahudhuria shule ya kati, wanamaliza katika miaka miwili. Mahali fulani njiani wanaweza kuanza kulifuasa kundi dogo la watoto—kuzidisha wafuasa wa wanafunzi!

- Agiza *Kumfuata Yesu* na vitabu vingine vya *Hatua Kuelekea Ukomavu* mtandaoni katika www.reach-out.org. Utataka kupata nakala yako mwenyewe ya *Kumfuata Yesu*. Kipitie kama vile watoto wanavyopitia vitabu vyao.
- Amua na kikundi chenu wakati, mahali, muda wa mkutano na idadi ya wanakikundi. Idadi nzuri ni kutoka kwa watu wanne hadi nane. Kila kitabu huchukua angalau wiki kumi kukamilika.

**6. Ongoza**. Mafanikio ya kikundi hayategemei sana mtaala, bali juu ya jinsi unavyoongoza. Jenga mahusiano.
Watie wanafunzi wako umakini. Fuata miongozo hii ili kuunda kikundi.

- *Andaa*. Katika nyakati hizi, watu wamekua na tabia ya kutojiandaa. Unaweza kuwasaidia kuja wakiwa wamejitayarisha kwa kuwapigia simu siku chache kabla ya mkutano kuwauliza ikiwa wamefanya kaizi-ziada. Ikiwa hawajajiandaa, waulize kama wanahitaji msaada. Ikiwa ndiyo, pitia kazi pamoja nao. Ikiwa wanakuja bila kujitayarisha, kutana nao kibinafsi wakati wa juma ili kuwasaidia kujitayarisha. Fanya hivi mpaka wapate mazoea.
- *Zingatia*. Anza kila mkutano kwa kuwakumbusha madhumuni ya kikundi. Kariri Mathayo 4:19 na msemezane kila wiki mkikariri.
- *Rejelea*. Kwa wiki mbili za kwanza, pitia ahadi kwenye ukurasa wa 11 wa *Kumfuata Yesu*. Wakumbushe tena waje wakiwa tayari. Kila juma waombe warudie umaizi mmoja mahususi ambao Mungu aliwafundisha juma lililopita na njia moja mahususi waliyotumia ufahamu huo.
- *Omba*. Baada ya kuwakumbusha juu ya madhumuni yao na kupitia utambuzi wao, wagawe katika sehemu tatu za maombi. Waweke katika vikundi sawa vya watu watatu kwa wiki kadhaa, kisha uwabadilishe. Ikiwa kikundi hakigawanyiki hasa katika watatu, ombeni wawili wawili.
- *Jadili*. Tumia angalau dakika thelathini hadi arobaini kupitia nyenzo zinazohusiana na kitabu. Wanapoibua mada nje ya mjadala makini, washirikishe, lakini usipotoshwe. Jadili mada hizo baadaye. Wakati huo huo wahimize kuzungumza. Zuia kishawishi cha kutoa mihadhara. Waache wao wazungumze zaidi.
- *Shiriki*. Tenga muda kila juma ili kuzungumzia masuala ya kibinafsi na maswali yanayozushwa. Mara ya kwanza mazungumzo yatakuwa ya kijuujuu, lakini kadiri kundi linavyozidi kuwa karibu watajadili masuala yao ya ndani na kwa uwazi. Iwapo muda utakuwa tatizo, waalike wakutane nje ya muda wa kikundi ili kuendelea.
- *Husisha*. Mara kikundi kinapoanza, washirikishe katika kufanya huduma nje ya kikundi — kukidhi hitaji, kumshiriki Kristo na marafiki zao, kwenda vitongojini, kufanya mkutano wa kimisheni wa ndani, au kufanya safari ya kimisheni ng’ambo.

Unapozifuata hatua hizi, Bwana atakutumia pamoja na kundi lako na wale wanaowashawishi kwa njia ambazo huwezi hata kufikiria sasa!